

Swahili transcript:

Nicholaus: Halafu kitu kingine ni kwamba, ukiangalia watu wengi kwamba anasema anasoma ili aajiriwe, yaani kwamba kuna ile ni kama dhana kwamba nikisoma ni lazima niajiriwe. Sasa ukiangalia kwamba kwa sababu uchumi wetu unakua, kwamba nafasi za kazi ni chache kuliko watu watakaomaliza chuo. Lakini kwa sababu uchumi unakua, tuna nafasi kubwa ya kutengeneza ajira mpya. Sasa ukiangalia kwamba elimu labda ule msukumo wanaopewa watu wakiwa labda chuoni ama sekondari ukiangalia kurudi nyuma, je kuna msukumo wa kutosha kuonyesha watu kwamba kazi ikikosekana wakati mwingine inabidi utengeneze ajira mwenyewe ama?

Fortunatus: Huo msukumo haupo, kwa sasa hivi kuna hii sera ambayo imewekwa, sera ya...hii entrepreneurship, sera ya ujasiliamali, yaah! mambo ya ujasiliamali inafundishwa, imewekwa sasa hivi. Lakini sasa waligundua kwamba hii sera haitafanya kazi kama mtu ukimpa sasa hivi hiyo sera kwamba anza sasa hivi mambo ya ujasiliamali kama hujaiweka kuanzia chini, unaona? Kwa hiyo walipogundua hiyo kitu, sasa hivi wanataka kuanza kuifundisha kuanzia chini, kwamba kuanzia watu walio shule ya msingi waanze kufundisha mambo ya ujasiliamali na nini, lakini kwa huko nyuma ilikuwa haipo hii kitu, sawa? Kwa hiyo hata sasa hivi hii kazi imeshindwa kufanya kazi na ndio maana wameona waanze tena chini waje juu. Unajua hili tatizo la zamani, zamani ilikuwa ni kwamba wazazi wetu akiwa yuko chuo, akiwa bado yuko chuo bado anaendeleo kusoma lakini tayari chance yake ya kufanya kazi katika kampuni inakuwepo, yaani tayari ana kazi tayari kwenye kampuni. Kwa hiyo watu wengi tumekua katika hiyo kwamba tutapata tu ajira, tutapata tu ajira. Lakini sasa hivi tumekuja kukugundua kuwa hapana, mtu anaweza akaanzisha kampuni, akaanzisha biashara, akaanza kufanya nini akaanza kufanya kazi mwenyewe na yeye akaajiri watu, umeona eeh? Lakini kama nilivyokuambia hiyo sera haifanyi kazi vizuri mpaka uanzie chini.

Andrew: Nadhani pia ukiangalia kiutamaduni, jamii zetu yaani za kitanzania sio wafanya biashara sana, wengi wamekuwa ni wakulima kuanzia siku za nyuma. So, lile wazo tu kwamba nianzisha biashara, biashara mara nyingi watu wanafanya kama *last resolution*, kwamba hana jinsi tena ya kuishi imebidi afanye biashara, lakini huu utamaduni haukuwepo kuanzia nyuma. Kwa hiyo hata ile legacy ya kwamba tumeachiwa na wazazi kutoka yaani kwa wazazi wao, sanasana lazima labda watafundisha kitu kidogo kuhusu ukulima. Hata mimi nyumbani kuna shamba, nini, hata kama kitu kingine kitanishinda, *definitely* najua nitalima, najua mahindi yanakuwa hivi, kuna kupalilia, kuna kuweka mbolea, najua hilo yaani kwamba kitu ambacho kipo, eeh!. Kwa hiyo kama sasa hivi nikisema niaanzisha biashara, naweza nikamfuata mzazi wangu pengine hata asiwe na wazo kwamba hatufanyi hivi, fanya hivi. Kwa hiyo biashara sawa inaonekana ni jambo muhimu lakini huo msukumo bado kwa watu wengi ni jambo ambalo bado hawana.

English translation:

Nicholas: Many people say they study so that they can be employed somewhere. They have the attitude that they should be employed somewhere. As we know our economy is growing. Many people will be graduating from universities but there are few employment opportunities for them. Do you think there is a need to let people know when they are still in secondary schools or colleges that if they don't get employment after their studies, they can create their own businesses? What do you think about that?

Fortunatus: There is no emphasis on self-employment. There is an entrepreneurship policy, but they forgot to establish this policy in primary schools. That's why they want to teach this policy now in the primary schools. People can learn when they are still young. It is not easy to tell people to practice entrepreneurship if they don't have the knowledge and skills of doing it. This policy is new; it was not like this before. When our parents went to college, they knew for sure they would be working in a certain company. There was already an opportunity to be employed somewhere. That's why many people have this mentality that they will get employment somewhere. But now we have come to realize that anyone can establish a company or start a business and can employ other people. You see? As I said, this policy doesn't work unless you start at the primary school level in training people while they are young. When they grow up, they will be able to practice entrepreneurship.

Andrew: It is not our culture to do business. Many Tanzanians are not business men or women; many are farmers. Even the idea of doing business most of the time comes as a final solution. A person might not have anything to sustain his life, so a business is something that will help him manage his life. This way of life was not there in the beginning. Most of the time parents can teach their children about agriculture. Even me, I have a farm plot at home. If it works out the way I want, I will definitely grow maize, because I know how to grow maize. I will do the weeding and apply fertilizer to get good crops.

If I want to start a business, and I will go and ask my parents, but they will not have an answer or advice about what I should do. They are not familiar with business. So while business seems to be important, many people do not see it as a big deal.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.